**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...!**

Tumekutana leo kwa ajili ya mambo matatu muhimu yanayohusu uimarishaji wa afya zetu, ambayo ni uanzishwaji wa huduma ya upandikizaji mimba, uwashaji wa vifaa vya kusaidia kusikia kwa watu wenye changamoto ya kusikia na kupokea magari maalum ya kutolea huduma za afya. Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Afya na Uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kumualika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii, lakini kutokana na majukumu mengi aliyonayo hakuweza kushiriki nasi. Hivyo, amenituma kumwakilisha.

**Ndugu Wananchi,**

Napenda kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuimarisha na kuboresha huduma za afya nchini, kwa kuimarisha upatikanaji wa vifaa tiba, wataalamu na dawa, pamoja na kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya. Jitihada hizo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025 (Ibara ya 83 (a)) ili kujenga Taifa lenye afya na nguvukazi imara na yenye tija. Katika azma hiyo, Serikali imeongeza Bajeti Wizara ya Afya kutoka Shilingi bilioni 900.1 mwaka 2020/21 hadi Shilingi trilioni 1.3 mwaka 2024/25. Katika kipindi hicho, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya afya iliongezeka kutoka 40% ya bajeti ya afya mwaka 2020/21 hadi 59% mwaka 2023/24 na katika mwaka huu wa fedha inakadiriwa kufikia 52%. Aidha, katika kukabiliana na upungufu wa wahudumu wa afya, Serikali ilitoa vibali vya ajira zipatazo 13,187 katika mwaka wa fedha 2023/24.

**Ndugu Wananchi**

Uzinduzi wa huduma za upandikizaji mimba na vifaa vya usikivu ni hatua muhimu sana katika kusaidia wananchi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya uzazi na watoto waliozaliwa wakiwa na changamoto ya usikivu. Ni faraja kuona huduma ya upandikizaji wa mimba sasa itaanza kutolewa kwa mara ya kwanza nchini katika Hospitali ya Umma. Awali huduma hizi zilipatikana katika hospitali za binafsi pekee. Vilevile, huduma hii ya upandikizaji mimba, licha ya kutolewa na vituo binafsi hapa Dar es salaam na Arusha, wananchi wengi walilazimika kutafuta huduma hiyo katika nchi za nje kama vile Uturuki, Afrika Kusini na Kenya. Hivyo, natoa pongezi nyingi kwa Wizara ya Afya, Bodi ya wadhamini, Menejimenti, Madaktari na Wataalam wa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kuanza mradi wa huduma ya kupandikiza mimba. Nimeambiwa kuwa mradi huu ulianza mwaka 2019 na nimejionea mwenyewe kuwa umetekelezwa kwa viwango vya kuridhisha. Aidha, nawapongeza pia kwa kutekeleza mradi huu kwa kutumia fedha za mapato yenu ya ndani (Sh. 1.2 Bilioni). Hatua hii ni mfano wa kuigwa na unaopaswa kuendelezwa.

Nimefahamishwa kwamba, kabla ya mwaka 2017 huduma ya kusaidia usikivu (Cochlear Implant) ilikuwa haipatikani hapa nchini na iliwalazimu wenye changamoto ya kusikia kupelekwa nje ya nchi ambapo gharama za matibabu ni kubwa. Ninafurahi kuwa kwa sasa huduma hii inatolewa na wataalamu wetu wa ndani na hivyo kupunguza gharama za matibabu. Hatua hii ya Hospitali ya Taifa Muhimbili ni utekelezaji wa azma ya

Serikali ya kupunguza idadi ya wagonjwa wanaokwenda kutibiwa nje ya nchi kutokana na upungufu wa wataalamu bobezi au ukosefu wa vifaa vya kutolea huduma husika.

Kipekee, naipongeza kwa dhati timu ya wataalamu iliyoshiriki katika kufanikisha kutoa huduma za kibobezi kwa Watoto hawa ambao wameingia katika hatua mpya ya maisha yao ya kuweza kusikia. Vilevile, nawaomba sasa wataalam wetu mfikirie kuhusu msaada zaidi wanaohitaji watoto hawa, hususan kwa hatua zile ambazo hawakuzipitia kutokana na kushindwa kusikia, kama vile kuwasaidia kujifunza kuzungumza (speech therapy n.k.).

**Ndugu Wananchi,**
Serikali ya awamu ya sita imeweka kipaumbele katika kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi. Katika kutekeleza hilo, imewekeza katika ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya, rufaa na kanda. Aidha, upatikanaji wa huduma za afya karibu zaidi na wananchi unawezeshwa pia na kuanzishwa kwa huduma za afya zinazotembea (mobile clinics), ambapo wataalam wa aina mbali wanajumuika pamoja kutoa huduma katika eneo husika.

Katika hili, napenda kumshukuru kwa dhati Bi. Alisha Moopen, Mkurugenzi Mtendaji wa Aster DM Healthcare FCZ, kwa kuiwezesha Hospitali yetu ya Taifa Muhimbili kusogeza huduma za afya kwa wananchi. Msaada wa magari haya (mobile clinics) hakika utasogeza huduma kwa jamii ambazo bado ziko mbali na vituo vya kutolea huduma lakini pia utasaidia kuboresha utoaji huduma za afya. Huduma hii itawezesha Hospitali yetu ya Taifa Muhimbili kupeleka madaktari na watalaam waliobobea kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu, kulingana na aina ya wagonjwa na huduma inayohitajika. Natoa wito kwa wadau wengine kusaidia katika eneo hili.

**Ndugu Wananchi,**
Sambamba na uwekezaji mkubwa unaolenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na kibobezi, Serikali imedhamiria kutekeleza kwa vitendo ajenda ya kimkakati ya kukuza utalii wa tiba hapa nchini ili kuliongezea Taifa fedha za kigeni na kuchochea ukuaji wa Pato la Taifa kupitia sekta ya huduma. Hivyo, kuzinduliwa kwa huduma hii ya upandikizaji mimba na upasuaji wa kupandikiza vifaa vya kusaidia kusikia, kumepanua wigo wa utalii wa tiba hapa nchini.

Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kutilia mkazo masuala machache yafuatayo: **Kwanza,** ni kuhusu umuhimu wa kuvitunza kwa umakini vifaa hivi vya kisasa vilivyopatikana kwa gharama kubwa ili vitumike kutoa huduma bora na vitusaidie kwa kipindi kirefu kijacho. **Pili,** Ili kuufanya uwekezaji huu kuwa endelevu, ni muhimu kuondokana na utegemezi wa wataalam kutoka nje. Jitihada za makusudi ni lazima zichukuliwe ili kuwezesha uhamishaji wa teknolojia (technology transfer) na ubunifu (innovation). Wizara ya Afya iandae mpango madhubuti wa kuwajengea uwezo wataalam wetu wa ndani watakaoweza si tu kuvitumia bali hata kuvifanyia ukarabati vifaa vyote vya kisasa, pindi hitaji hilo litakapojitokeza. **Tatu,** nawasihi Watanzania kuchangamkia huduma zitolewazo na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambazo ni bora na zenye gharama nafuu. **Nne,** taarifa kwa umma kuhusu upatikanaji wa huduma hizi za

kibingwa hapa Muhimbili itolewe ili wananchi wenzetu, na wengine kutoka nchi jirani, wenye changamoto mbalimbali za ugumba na usikivu waweze kujitokeza kupata huduma.

**Ndugu Wananchi,**

Kwa kumalizia, nimepokea maombi ya msamaha wa kodi kwenye vifaa tiba muhimu katika huduma ya upandikizaji mimba ili kusaidia kushusha gharama za huduma hiyo. Hivyo, ninamtaka Waziri wa Afya kukutana na Waziri wa Fedha ili kuona namna bora ya kutekeleza pendekezo hilo.

Baada ya kusema hayo, sasa nipo tayari kuzindua rasmi huduma ya upandikizaji mimba (IVF) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ambayo ni hospitali ya kwanza ya umma kutoa huduma hizi nchini. Vilevile, kuwasha rasmi vifaa vya kusaidia kusikia kwa watoto (Cochlear implant) hawa 14 walionufaika na upasuaji wa kupandikiza vifaa hivyo.

**Mungu Ibariki Afrika...Mungu Ibariki Tanzania**
**ASANTENI SANA KUNISIKILIZA**